

IGP SIRRO AWAVALISHA NISHANI MAOFISA, WAKAGUZI NA ASKARI 123

Na Demetrius Njimbwi

Januari 21, 2022 Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, aliwavalisha nishani maafisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali 123 waliotunukiwa nishani na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Akisoma taarifa ya kuvisha nishani hizo, Mkuu wa Operesheni Maalum za Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Mihayo Msikhela, amesema kuwa, Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa mamlaka aliyopewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Shughuli za Rais, Sura ya 9 toleo la urekebu la mwaka 2002 kama ilivyotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 803 la tarehe 03 Desemba 2021 na Taarifa ya kawaida Na. 2229 ya tarehe 03 Desemba 2021, amewavalisha maafisa, wakaguzi na askari hao nishani ya miaka 60 ya uhuru, nishani ya utumishi uliotukuka na nishani ya utumishi mrefu na tabia njema.

SACP Mihayo amesema kuwa miongoni mwa waliotunukiwa nishani ya miaka 60 ya uhuru ni pamoja na maafisa 5 akiwemo Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Nyakoro Sirro, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo (CP) Liberatus Sabas, Kamishna wa Zanzibar (CP) Mohamed Hassan, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Maria Nzuki na Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Paul Sanga.

Nishani hii imetunukiwa kwa majeshi ya ulinzi na usalama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo imetolewa kwa maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Maafisa, Wakaguzi na askari wa Jeshi la Polisi Tanzania, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Kwa upande wa Nishani ya Utumishi Uliotukuka, SACP Mihayo amesema jumla ya maafisa, wakaguzi na askari 58 miongoni mwa waliotunukiwa nishani hiyo ni pamoja na Kamishna wa Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii (CP) Dkt. Mussa A. Mussa, Naibu Kamishna wa Polisi Mstaafu (DCP) Sospeter Kondela na Kamishna

Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) David Misime, walivishwa nishani hiyo ambayo hutunukiwa kwa maafisa walio kwenye utumishi hai wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wa cheo cha Meja kwenda juu na wale wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa cheo cha Mrakibu au wa juu ya cheo hicho na Maafisa Waandamizi wa Idara ya Usalama wa Taifa ambao wametimiza miaka ishirini mfululizo ya kuwa afisa.

Vilevile, Nishani ya utumishi mrefu na tabia njema ilivalishwa kwa maafisa na wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali 60 ambapo sifa ya nishani hii ni kuwa hutunukiwa kwa maafisa wasiokuwa na nyota walio katika utumishi hai wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania na Wakaguzi, Wakaguzi Wasaidizi, Sajeni Taji, Sajenti na Koplo wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji waliotumikia Jeshi hilo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano katika vyeo hivyo na watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa ambao wametumikia Idara hiyo mfululizo kwa kipindi hicho na tabia ya kuweza kusifika.

Kuvalishwa kwa nishani hizo kumetokana na Mhe. Rais kuwatunuku nishani maafisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali kwenye maadhimisho ya sherehe za miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Hafla za uvalishaji wa nishani hizo zilifanyika kwenye viwanja vya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi jijini Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiwemo Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, watendaji wengine wa serikali pamoja na askari wa vyeo mbalimbali.